بسم الله الرحمن الرحيم

26/Safar/1427H=26March/2006 AD.Madinatul Rasuul s.a.w.-Saudi Arabia.
Makala namba 4.

# HII NDIYO DAAWA YETU

## JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

## UHARAMU WA KUYAJENGEA MAKABURI.

Amesema Swahaba mtukufu Jabir bin Abdillahi r.a;
**:((نهى رسول الله صلى الله عليه وسلم أن يجصص القبر وأن يقعد عليه وأن يبنى عليه)).**
[Amekataza Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w
kulipaka chokaa kaburi,na kulikalia,**na kulijengea** ].
Tazama sahihi muslim juzuu 3ukurasa62.

MUANDISHI;

ABUL FADHLI QASSIM MAFUTA QASSIM.

بسم الله الرحمن الرحيم

## UTANGULIZI

Mnamo tarehe 10/Shawaal/1426H =12/Nov/2005M,niliipata makala iliyotolewa na vijana wa msikiti wa kwa mnyamani Buguruni - Dares salaam.

Makala hiyo imeelekezwa kwa Sheikh Juma poli,makala hiyo inaonekana ina zaidi ya miaka mitatu tangu tarehe niliyoipata,kwa mujibu wa maneno ya aliyenipa.

Makala hiyo inaonekana wazi kuwa imeandikwa na watu ambao si wasomi wa dini,wakishirikiana na watu ambao wanadhaniwa kuwa ni wasomi wa dini,
na hali ya kuwa si wasomi bali ni wababaishaji,kama ilivyo kawaida katika jamii yetu akijitokeza mtu na aya mbili tatu akajua kuzitafsiri,na akawa na ufundi wa kugeuza geuza maneno basi tayari naye ni msomi na ana wafuasi!!

Na ishara za wazi zinaonyesha kuwa muandishi/waandishi wa makala hii si wasomi,ni ule upotoshaji wa haki wa dhahiri ambao umejaa kwenye makala hiyo,na pia makosa ya kielimu ambayo yanadhihirisha uduni na uchache wa eilimu ya dini kwa waandishi hao,
kama vile kukosea majina ya wanawachuoni mashuhuri kabisa katika uislamu, tafsiri za makosa za maneno ya wanawachuoni ambazo zina pelekea kupotosha maana walizo kusudia,na kutoa fat'wa ambazo ni kinyume na fat'wa za maulamaa wakubwa,na kutanguliza hamasa mbele kuliko hoja za kielimu,bila ya kujali athari mbaya itakayo jitokeza katika jamii kwasababu ya ujasiri wao wa kuyashupalia mambo wasiyo na ujuzi nayo,
na bila ya kuogopa kwamba wakifanya hivyo watakwenda kuulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya Qiyama.

Amesema Allah{s.w.t};

{وَلاَ تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ أُولـئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْؤُولاً }

[wala usifuate(ukipita ukiyasema au kuyafanya) usiyo na ilimu nayo.Hakika masikio na macho,na moyo vyote hivyo ni vyenye kuulizwa].
Surat Bani Israil aya 36.

Linalo nihusu mimi kwenye makala hiyo,ni zile fat'wa potofu,na data feki za kielimu,maana baada kuisoma makala hiyo ghera ya dini ilinishika na sikuweza kuuvumilia,na kuunyamazia upotoshaji huo ulio beba sura ya kuitetea dini,na ndiyo asili na chimbuko la makala hii iliyo mikonono mwako.

Kwa hivyo basi,tutataja katika makala hii;

-Hadithi za Bwana Mtume{s.a.w.} zinazo kataza kuyajengea makaburi,na hadithi za kuyavunja makaburi iwapo watu wamekhalifu makatazo hayo.

-Vilevile tutataja fat'wa za maulamaa wakubwa akiwemo Imamu Shaafy{r.a} juu ya hukumu ya kuyavunja makuburi yaliyo jengewa.

-Pia tutataja sababu za kukatazwa kuyajengea makaburi.

Mwisho tutataja majibu ya Hoja ambazo zimetolewa na waandishi wa makala hiyo hoja ambazo zina halalisha kuyajengea makaburi.

## HADITHI SAHIHI ZA MTUME S.A.W. ZINAZO KATAZA KUYAJENGEA MAKABURI NA KUAMRISHA KUYAVUNJA;

Kwanza kabisa ndugu yangu muislamu napenda ujue kwamba maneno ya Bwana Mtume {s.a.w.} ni wah'yi unaotoka kwa Allah s.w.t.
hivyo basi hatamki kwa matakwa na matamanio ya nafsi yake.
Amesema Allah{s.w.t.};

{إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَى *وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَى

[Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake).Hayakuwa hayo anayo yasema ila ni ufunuo unao funuliwa kwake)
AnNajmi aya3-4.

Na pia nitapenda ufahamu kwamba muda wa kuwa umekubali kuwa muislamu huna hiyari yakuchagua -lipi nalitaka nilifanye nalipi silitaki -mbele ya hukumu ya Allah s.w.t. na Mtume s.a.w.
Amesema Allah s..w.t;

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْراً أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ
وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالاً مُّبِيناً

[Haiwi kwa muumini mwanamume wala muumini mwanamke anapo hukumu Mwenyezi Mungu,na Mtume wake jambo lolote kuwa na hiari katika jambo lao…].
Al ah'zab aya ya 36.

Pia amesema Allah{s.w.t.};

{وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ }

[Na kile alicho kupeni mtume kichukueni,na kile alicho kukatazeni komeni (kiwacheni) na muogopeni mwenyezi mungu hakika mwenyezi mungu ni mkali wa kuadhibu].
Suratul Hashir aya ya7.

Na miongoni mwa mambo aliyo yakataza Bwana Mtume {s.a.w} ni kuyajengea makaburi pale aliposema Swahaba mtukufufu Jabir bin Abdillahi r.a;

عن جابر رضي الله عنه قال :

:((نهى رسول الله صلى الله عليه وسلم أن يجصص القبر وأن يقعد عليه وأن يبنى عليه)).

[Amekataza Mtume wa Mwenyezi Mungu{s.a.w}
kulipaka chokaa kaburi,na kulikalia,na kulijengea (1)].

Amesema Imamu Swan'any alipokuwa akiisherehesha hadithi hii;

[Hadithi hii ni dalili juu ya uharamu wa mambo matatu yaliyotajwa,kwasababu ndiyo asili ya makatazo..](2)

Hayo ni makatazo ya mtume {s.a.w} kuhusu kuyajengea makaburi.

Na ilivyo katika qawaaid (misingi) ya eilimu ya usulul fiq'hi ni kwamba asili ya makatazo huwa yana fahamisha uharamu wa hilo jambo lililo katazwa,mpaka ipatikane hoja na dalili nyingine kama hiyo au iliyo na nguvu zaidi kuliko hiyo itakayo fahamisha kinyume chake.

---

(1)Tazama sahihi muslim juzuu 3ukurasa62.
Na Sunan Abi Dawdi juzuu 2 ukurasa 71.Na Sunan Tir'midhy juzuu 2 ukurasa155.
Na Sunan Nnasai juzuu 1 ukurasa 284-285.Al mustad'raq juzuu 1 ukurasa370
(2)Tazama subulus salaami 2/176-177.

Kwahivyo basi ni haramu kuyajengea makaburi kwa kutopatikana hoja na dalili yenye nguvu ya kuigeuza hadithi hii,na kama ipo aya au hadithi nyingine inayo sema kinyume cha katazo hili -na wala hawatoipata-basi tuelezwe.

Na iwapo ndugu muislamu umelijengea kaburi la maiti wako basi ujuwe kwamba umefanya makosa kwa mujibu wa sheria ya kiislamu,
na wajibu wako ni kutubia kwa Mwenyezi mungu kwa kulivunja kaburi hilo,na kufanya hivyo siyo kumdhalilisha maiti wako,bali ni kuifuata amri ya mtume s.a.w kipenzi chako mbora wa viumbe wote.

Imepokewa kutoka kwa Abul Hayyaj Al asady amesema;
Aliniambia mimi Ally bin Abi Twalib;

[Je nikutume kwa jambo ambalo alinituma mtume wa mwenyezi mungu {s.a.w}?

(Usiliwache sanamu lolote ila umelivunja,wala kaburi lolote lililonyanyuka ila umelisawazisha].

Amesema Imamu An nawawy;
[..linatiliwa nguvu -suala la-kuvunja (makaburi) na kauli ya Mtume{s.a.w}; usiliwache kaburi lililo nyanyuka juu ila umelisawazisha..].

---

1)Tazama sahihi muslim Hadithi namba 969.na Sunan Abi Dawd Hadithi namba3218.
Na Sunan Tir'midhy Hadithi namba1049.na Sunan Nnasai 4/88,89.
Na wameisahihisha Hadithi hii maimamu hawa muslim,Imamu Tir'midhy,na Al muhaddith Al Albany.

2) Tazama shar'hu muslim ya Nnawawy 3/41.

Na amesema Imamu As shawkany katika kitabu chake shar'hus sudur alipokuwa akiisherehesha hadithi hii;

[ katika hadithi hii kuna ushahidi mkubwa wa kulisawazisha kila kaburi lililo inuka juu zaidi ya kiwango chake cha kisheria,tena kwa lazima-si hiari- na miongoni mwa sampuli za kuinuka kaburi,ni kuinuka kimo chake,na kuweka juu yake kuba au msikiti kwasababu hayo yote yamekatazwa bila shaka yoyote wala utata,na kwasababu hiyo Mtume s.a.w. alimtuma Ally r.a. kuyavunja makaburi…].(1)

Kwa hiyo ndugu muislamu,hayo ndiyo mafundisho sahihi ya uislamu juu ya suala zima la kujengea makaburi,ni kwamba haifai kuyajengea makaburi.

Na kama kuna watu walikuwa hawajui wakafanya kosa hilo bila ya kujua basi makatazo haya yakiwafikia kinachotakikana kwao ni kuyavunja makaburi hayo,kwa ajili ya kuitekeleza na kuienzi amri ya Sayyid'na Muhammad s.a.w.

Na katika mambo kama haya ndiyo unabainika upeo wako wa kumpenda mtume s.a.w na si mapenzi ya kuimba,na kupiga ngoma, na kucheza,kisha ukadai kwamba unampenda Bwana Mtume s.a.w.

Ama kwenye amri na makatazo yake unayatupilia mbali bila ya kujali, hapana!
Hayo ni mapenzi ya urongo,na inaonyesha wazi kwamba wewe unapenda ngoma tu,kwani hakika mwenye kupenda humtii yule ampendae.

---

(1)Tazama shar'hus suduri fi tah'riimi raf' il quburi ukurasa 55.

<u>FAT'WA ZA ULAMAA JUU YA KUYAJENGEA MAKABURI;</u>

Hebu sasa tuangalie fat’wa za wanawachuoni wetu, je na wao wanatuambia nini kuhusu kuyajengea makaburi?

Tunaanza na fatawa za maulamaa wa kishaafy;

**1-kwanza kabisa ni Imamu Shaafy mwenyewe r.a**
Amesema Imamu Shaafy r.a;

[Niliwaona baadhi ya watawala katika mji wa Makka wakiyavunja yale yaliyojengewa katika makaburi,na sikuwaona wanawachuoni wa fiq’hi wakiwasema vibaya kwa hilo..].

**2-Imamu Ar Raafy;**
**Amesema Imamu Ar Raafy Al shaafy r.a;**

[Na kama kaburi litajengewa basi livunjwe,ikiwa sehemu ya makaburi ni waq’fu..)).

**3-Imamu An Nawawy;**
**Amesema Imamu An nawawy {r.a};**

[Na wamesema wenzetu (katika madhehebu)Allah awarehemu;na hakuna tofauti kati ya kujengwa kuba au nyumba au kitu kingine.

Kisha itaangaliwa kama sehemu ya kuzikiwa ni ya wak’fu basi ni haramu hilo(jambo la kujengea) na wamesema wenzetu kuwa;litavunjwa jengo hilo,na hakuna tafauti(kati yao).

---

(1) Tazama al Ummu ya Imamu Shaafy 2/160.
(2) Tazama al aziz shar'hul wajiz 2/452.
(3) Tazama al maj'muu ya An nawawy 5/189.

**4-Imamu Zakariyyal Answaary;**
**Amesema Imamu Zakariyyal Answaary Ashaafy;**

[Na ni haramu kujengea katika makaburi ya wak'fu,ikiwa ni ada ya watu wa mji kuzikiana mahali hapo…}.(1)

Amesema tena;

[Na kama(kaburi)litajengewa katika sehemu hiyo basi litavunjwa..].(1)

Hizi tulizo zitaja hapa ni baadhi ya fatawa za maulamaa wakubwa wa kishaafy akiwemo Imamu Shaafy mwenyewe r.a. na hakuna shaka kwamba wao si mawahabi.

Kwahiyo kazi kwenu enyi mnaojiita mashaafy,sasa hizo ndiyo fatawa za Imamu na wafuasi wake wakubwa ,je mko tayari kuyavunja makaburi ya maiti zenu?

Lakini mimi nina wasiwasi mkubwa sana huwenda mkazitupilia mbali fatawa hizi za mwanawachuoni huyu bila ya kujali,maana nyinyi hamuwachi kupingana naye kila uchao,hata kama atatoa hoja na dalili lakini yakishapingana na mas'lahi yenu ushaafy basi tena.

Na mfano mzuri ni katika suala la khitima na kuzipeleka thawabu za kisomo cha Qur'an kwa maiti.
Imamu Shaafy amesema kuwa maiti hanufaiki chochote na matendo hayo lakini mlipoona kwamba jambo hilo linapingana na mas'lahi yenu mkamtupilia mbali Imamu Shaafy na ushaafy wake,mkabaki na ushafy wa kuQunuti katika swala ya al fajiri tu,

kwahiyo katika suala hili pia nina wasi wasi linaweza likajitokeza jambo kama hilo,ila kwa wale wanao taka kujua ukweli na kuufuata.

---

4-Tazama fathul wahaab shar'hu man'hajit tullaabi

**Pili ni fatawa za Ulamaa wasio kuwa wa kishaafy;**

**1-Imamu Ibnul Qayyim;**

**Amesema Imamu Ibinul Qayyim Al jawziyyah r.a ;**

[..Na hali kadhalika makuba yaliyojengwa juu ya makaburi, yanapasa kuvunjwa yote,kwasababu yameasisiwa kwa kumuasi mtume{s.a.w},kwasababu yeye amekataza kuyajengea makaburi…](1)

Amesema tena;

[Kuvunja makuba,majengo,na misikiti iliyojengwa juu ya makaburi ni jambo bora,kwasababu mtume{s.a.w} ame walaani wenye kuijenga misikiti juu yake,na amewakataza kuyajengea,kwa hiyo ni wajibu kufanya haraka,na kuwasaidia kuyavunja yale ambayo mtume{saw}amewalaani watendaji wake..](1)

**2-Imamu Swan'aany;**

**Amesema Imamu Swan'aany alipokuwa akiisherehesha Hadithi ya Jabir{r.a}tuliyoitaja;**

[Hadithi hii ni dalili juu ya uharamu wa mambo matatu yaliyotajwa,kwasababu ndiyo asili ya makatazo..].(2)

**3- Imamu Shawkaany;**

**Amesema Imamu Shawkaany alipokuwa akiisherhesha Hadithi ya Allya{r.a.} tuliyoitaja;**

[katika hadithi hii kuna ushahidi mkubwa wakusawazisha kila kaburi lililo inuka juu zaidi ya kiwango cha kisheria,tena ..

---

(1)tazama Ighathatul lah'faan ukurasa 185.
(2)tazama subulus salaami 2/176-177.

..kwa ulazima,na miongoni mwa sampuli za kuinuka kwa kaburi,ni kuinuka kimo chake,na kuweka juu yake kuba,au msikiti,kwasababu hayo yote yamekatazwa bila ya shaka yoyote,wala utata,na kwasababu hiyo,mtume {s.a.w} alimtuma Ally{r.a}kuyavunja makaburi..].(1)

Bila shaka maulamaa hawa nao pia si mawahabi.

Kwahiyo ndugu yangu muislamu,kwa mujibu wa fatawa hizi za Ulamaa hawa tuliowataja akijitokeza mtu akikwambia kwamba mawahabi (Ah'lusunna wal jamaa) wanapinga kujengea makaburi,bila shaka unalo la kumjibu.

Na akikwambia kwamba;Mawahabi hawayaheshimu makaburi ya mawalii,na masharifu,ndiyo maana wanataka yavunjwe,bila shaka pia utakuwa na la kumjibu.

## KWA NINI MAKABURI YAVUNJWE?

Wanawachuoni wakubwa wa kishaafy wanatujibia swali hili;

**1-Amesema An nawawy;**

[Hakika amekataza mtume{s.a.w} kulifanya kaburi lake,na la mwingine kuwa msikiti,kwasababu ya kuogopea kupetuka mipaka katika kuliadhimisha,na kufitinika nalo,na huwenda hilo likapelekea kwenye ukafiri,kama ilivyo jiri kwa wengi katika umma zilizo pita].(2)

---

*(1)tazama Shar'hus Suduur fi tah'fimi raf' il Qubuur ukurasa 55.*
*(2)tazama shar'hu muslim 5/13*

**2-Na amesema Imamu Ibin Kathiri {r.a.};**

[Asili ya kuabudu masanamu,ni kupituka mipaka katika (kuyaadhimisha)makaburi,na watu wake].(1)

**3-Amesema Ar Raazy** baada ya kuelezea sababu zilizo waingiza watu waliopita kwenye ushirikina;

[Na mfano wao ni watu wa zama hizi,wengi hujishughulisha na kuyaadhimisha makaburi ya wakubwa wao,kwa kuitikadi kwamba wakiyaadhimisha makaburi yao,watakuwa ni waombezi wao mbele ya mwenyezi mungu'.(2)

Hebu sasa ndugu muislamu yatafakari maneno hao ya mtume {s.a.w} na hizi fatawa za wanawachuoni wote hawa,hivi kweli yale aliyo yaogopea mtume{s.a.w} kwa umma wake huu yametokea au bado?

-Je hakuna wanao yajengea makaburi? Je wako wapi hao na makatazo ya mtume{s.a.w}?

-Je hakuna wanaokwenda  makaburini kuabudu kwa kuweka nadhiri? Wakisema;sheikh mimi nikifanikiwa nitakufanyia kadha wakadha? Je huo ndio uislamu?

-Je hakuna wanaokwenda mkaburini kuomba kazi, watoto,na waume/wake?

Je hao ndio wakuombwa?amekwambia nani ukiomba kupitia kwa mabwana hao utakubaliwa?sasa je huu si ushirikina?

---

(1)-Tazama al bidayatu wan nihayat 10/703.
(2)-Tazama  taf'sirul kabir 17/63.

-Je hakuna wanao wazika maiti zao katika nyumba za ibada? kwani hivi kweli hasa hakuna sehemu za kuzikana ila misikitini ?au hawakuisikia kauli ya mtume s.a.w  isemayo;

[waovu katika watu ni wale wanao yaweka makaburi katika misikiti]?

Na hivi hawakuisikia kauli ya Mtume{s.a.w.} isemayo;

[msiyafanye makaburi kuwa ni misikiti,mimi nina kukatazeni hilo]?

Sasa wanasubiri nini wasiyaondoshe makaburi hayo? Ni kibri? Au wako tayari na lolote lile mbele ya Mwenyezi mungu siku ya Qiyama?Au ni udanganyifu wa baadhi ya wanaoitwa masheikh kwa kuwaambia eti hakuna neno?

Kwa ufupi ni kwamba haifai kuyajengea makaburi wala kuwazika maiti misikitini,na kama likitokea kosa hilo haraka sana linatakikana liondolewe, kinyume cha hivyo,wenye kuswali katika msikiti huo watapata dhambi na swala hazitoswihi - ukitoa msikiti wa mtume s.a.w kama tutakavyolielezea hilo katika makala ijayo- na hii ndiyo kauli iliyo na nguvu kwa wanawachuoni wa Ah'lis sunnati wal  Jamaa.

Pamoja na haya kuna baadhi ya masheikh wanao wababaisha watu wasiosoma,kwa kuwadanganya kuwa jambo hili lina faa! Ni mawahabi tu ndio wanao wakataza watu kufanya hivyo ! Basi masheikh hao wamuogope mwenyezi mungu.

Ndugu yangu muislamu mpaka hapa utakuwa umeufahamu upotoshaji ulio jaa katika makala iliyo tolewa na Sheikh wa msikiti wa kwa mnyamani Buguruni Dar es salaam,makala ambayo imejaa fatawa zilizo kinyume na mafundisho ya Mtume  s.a.w.na kinyume kabisa na kauli za maulamaa wakubwa wa kiislamu..!

فماذا تقوله النصحاء ؟*واذا ضلت العقول على علم

Fuatilia mfululizo wa makala zetu;

HII NDIYO DAAWA YETU JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIH

- **1,2,3.) Athari mbaya ya Uzushi katika uislamu.**

- **4,)Uharamu wa kuyajengea makaburi**
  (ni hii iliyo mikononi mwako).

- **5)Uharamu wa kuyajengea makaburi.**
  **Majibu na maelezo**

- **6)Uharamu wa kuswali kuelekea makaburi.**

Tanbihi;

1-Tafadhali usikose makala ifuatayo ni muhimu.

2-Ukiipata makala hii toa copy nyingine na umpe mwenzako kwa lengo la kueneza ujumbe

**وصلى الله وسلم وبارك على محمد وعلى آله وصحبه أجمعين.**
**وآخر دعوانا أن الحمد لله رب العالمين.**